

# Tanzania



Atlasi ya Malaria  
Ngazi ya Halmashauri



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# **Atlasi ya Malaria katika ngazi ya Halmashauri**


**Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,  
Jinsia, Wazee na Watoto  
Dodoma**

**Wizara ya Afya  
Zanzibar**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)  
Dodoma**

**Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS)  
Zanzibar**

**Agosti 2018**



# Utangulizi

---


Kazi ya kukokotoa viwango vya malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya Tanzania ilifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) - Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto – Tanzania Bara na Wizara ya Afya - Zanzibar.

Sampuli iliyotumika katika Utafiti wa Viashiria vya Malaria Tanzania wa mwaka 2017 iliweza kutoa kiwango cha Malaria hadi ngazi ya mkoa. Aidha, mbinu ijulikanayo kama “Small Area Estimation - Direct Method” ilitumika kupata viwango vya malaria katika ngazi ya Halmashauri. Taarifa zilizotumika ni pamoja na viwango vya malaria katika ngazi ya mkoa, idadi watoto chini ya miaka 5 kwa kila Halmashauri. Takwimu nyingine zilizotumika ni idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka 5 waliotembelea sehemu zinazotoa huduma za afya katika halmashauri.

Taarifa zaidi kuhusu ripoti hii inapatikana kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), S.L.P. 2683, Dodoma, Tanzania. Simu: +255 (0)26-2963822/3/4; Nukushi: +255 (0)26-2963828; Barua pepe: [dg@nbs.go.tz](mailto:dg@nbs.go.tz); Tovuti: [www.nbs.go.tz](http://www.nbs.go.tz).

*Picha iliyo juu ya Atlasi hii inaonesha Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Umy Mwalimu (Mb.) akimkabidhi chandarua chenye dawa ya muda mrefu Bibi Mwantum Mohammed baada ya kuzindua ugawaji endelevu wa vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu kwa akinamama wajawazito na watoto wenye umri wa mwaka mmoja mpango ambao unaendeshwa na Shirika la Johns Hopkins kupitia mradi wa “Vector Works” chini ya ufadhili wa USAID kupitia Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria. Kulia (nyuma ya Bibi Mwantum Mohammed) ni Mkurugenzi wa USAID Tanzania, Bwana Andy Karas. (Picha kwa hisani ya Michuzi Blog, 2018)*


**MKOA WA ARUSHA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Arusha ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki cha malaria ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha tofauti ya asilimia 0.1 hadi 0.2 ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Halmashauri za mkoa wa Arusha.




**MKOA WA DODOMA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Dodoma ni asilimia 0.6. Hata hivyo, kiwango hiki cha maambukizi ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha kuna tofauti ndogo ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 katika Halmashauri za mkoa wa Dodoma. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa (asilimia 1.3) na kiwango cha chini kipo katika Halmashauri ya Kondoa Mji (asilimia 0.1).

**MKOA WA DAR ES SALAAM**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Dar es Salaam ni asilimia 1.1. Kiwango hiki cha maambukizi ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha kuna tofauti ndogo ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 katika Manispaa za mkoa wa Dar es Salaam. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Manispaa ya Kigamboni (asilimia 1.8) na kiwango cha chini kipo katika Manispaa ya Ubungo (asilimia 0.7).

**MKOA WA GEITA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Geita ni asilimia 17.3. Kiwango hiki cha malaria ni kikubwa kwa zaidi ya mara mbili ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Ipo tofauti kubwa ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Halmashauri za mkoa wa Geita. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita (asilimia 22.4) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Halmashauri ya Geita Mji (asilimia 10.4).


**MKOA WA IRINGA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Iringa ni asilimia 2. Kiwango hiki cha malaria ni cha chini ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha tofauti ndogo ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Halmashauri za mkoa wa Iringa. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo (asilimia 3.6) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Manispaa ya Iringa (asilimia 0.2).



**MKOA WA KAGERA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Kagera ni asilimia 15.4. Kiwango hiki ni kikubwa takriban mara mbili zaidi ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha tofauti kubwa ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Halmashauri za mkoa wa Kagera. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo (asilimia 18.9) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Manispaa ya Bukoba (asilimia 3.5).

MKOA WA KATAVI  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Katavi ni asilimia 7.1. Kiwango hiki cha maambukizi ni takriban sawa na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha viwango vya maambukizi ya malaria kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano vinatofautiana baina ya Halmashauri za mkoa wa Katavi. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Halmashauri ya Nsimbo (asilimia 10.4) na kiwango kidogo kipo katika Manispaa ya Mpanda (asilimia 2.9).

**MKOA WA KIGOMA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Kigoma ni asilimia 24.4. Kiwango hiki cha maambukizi ya malaria ni kikubwa zaidi ya mara tatu ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Vile vile, kiwango hiki ni kikubwa zaidi ukilinganisha na mikoa mingine hapa nchini. Matokeo yanaonesha tofauti kubwa ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Kigoma. Kiwango cha juu ni asilimia 30.8 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko na kiwango cha chini kipo katika Manispaa ya Kigoma (asilimia 14.7).

**MKOA WA KILIMANJARO  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Kilimanjaro ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki cha maambukizi ya malaria ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha hakuna tofauti ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 katika Halmashauri za mkoa wa Kilimanjaro.


**MKOA WA LINDI**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Lindi ni asilimia 11.7. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha ipo tofauti ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Lindi. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi (asilimia 13.3) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Manispaa ya Lindi (asilimia 8.6).




**MKOA WA MANYARA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Manyara ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha hakuna tofauti ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Manyara.

**MKOA WA MARA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Mara ni asilimia 11.2. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Vile vile, matokeo yanaonesha tofauti kubwa ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Mara. Kiwango cha juu kiwango cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti (asilimia 15.4) na kiwango kidogo kipo katika Manispaa ya Musoma (asilimia 1.9).

**MKOA WA MBEYA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Mbeya ni asilimia nne (4). Kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Hata hivyo, matokeo yanaonesha tofauti kubwa ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Mbeya. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Busekolo (asilimia 10.7) na kiwango kidogo kipo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya yenye kiwango cha malaria cha asilimia 0.5.

**MKOA WA MTWARA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Mtwara ni asilimia 14.8. Kiwango hiki ni zaidi ya mara mbili ya wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha tofauti kubwa ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Mtwara. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba Mji (asilimia 19.5) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Manispaa ya Mtwara (asilimia 7.3).


**MKOA WA MOROGORO  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Morogoro ni asilimia 9.5. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha tofauti kubwa ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Morogoro. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga (asilimia 17.5) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Manispaa ya Morogoro (asilimia 2.6).




**MKOA WA MWANZA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO CHINI YA UMRI WA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Mwanza ni asilimia 8.1. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha tofauti kubwa ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Mwanza. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe (asilimia 15.7) na kiwango kidogo kipo katika Manispaa ya Nyamagana (asilimia 1.1).

**MKOA WA NJOMBE**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Njombe ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki ni cha chini ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Hakuna tofauti ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Halmashauri za mkoa wa Njombe.

**MKOA WA PWANI**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Pwani ni asilimia 5.3. Kiwango hiki cha maambukizi ya malaria kiko chini ya wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Hata hivyo, matokeo yanaonesha viwango vya malaria vinatofautiana baina ya Halmashauri za mkoa wa Pwani. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti yenye asilimia 7.6 na kiwango cha chini kipo katika Halmashauri ya Kibaha Mji (asilimia 0.8).

**MKOA WA RUKWA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Rukwa ni asilimia 1.8. Kiwango hiki cha maambukizi ya malaria ni cha chini ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Hata hivyo, matokeo yanaonesha viwango vya malaria vinatofautiana miongoni mwa Halmashauri za mkoa wa Rukwa. Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ina kiwango kikubwa cha maambukizi ya malaria cha asilimia 2.7 na Manispaa ya Sumbawanga ina kiwango kidogo cha maambukizi ya malaria (asilimia 0.2).


**MKOA WA RUVUMA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Ruvuma ni asilimia 11.8. Kiwango hiki cha maambukizi ya malaria ni kikubwa zaidi ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha viwango vya malaria vinatofautiana miongoni mwa Halmashauri za mkoa Ruvuma. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Halmashauri ya Namtumbo (asilimia 16) na kiwango kidogo kipo katika Halmashauri ya Mbinga Mji (asilimia 5).




**MKOA WA SHINYANGA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Shinyanga ni asilimia 6.1. Kiwango hiki cha maambukizi ya malaria kipo chini ya wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Hata hivyo, matokeo yanaonesha viwango vya malaria vinatofautiana miongoni mwa Halmashauri za mkoa wa Shinyanga. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu (asilimia 11.1) na kiwango cha chini kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu (asilimia 2.9).

**MKOA WA SIMIYU  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO CHINI YA UMRI WA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Simiyu ni asilimia 6. Kiwango hiki kipo chini ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Hata hivyo, matokeo yanaonesha ipo tofauti ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Simiyu. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi (asilimia 10.6) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu (asilimia 2.1).

**MKOA WA SONGWE  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Songwe ni chini ya asilimia 1. Kiwango hiki ni cha chini ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha hakuna tofauti ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Halmashauri za mkoa wa Songwe.

**MKOA WA SINGIDA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Singida ni asilimia 2.3. Kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha tofauti ndogo ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Singida. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi (asilimia 7.7) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida (asilimia 0.3).


**MKOA WA TABORA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Tabora ni asilimia 11.7. Kiwango hiki cha maambukizi ni kikubwa zaidi ya wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha viwango vya malaria vinatofautiana miongoni mwa Halmashauri za mkoa wa Tabora. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua (asilimia 16.8) na kiwango kidogo kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga (asilimia 5.6).




**MKOA WA TANGA**  
**KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mkoa wa Tanga ni asilimia 3.1. Kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha ipo tofauti ya viwango vya maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri za mkoa wa Tanga. Kiwango cha juu cha malaria kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni (asilimia 5.9) na kiwango kidogo cha malaria kipo katika Halmashauri za Wilaya za Bumbuli na Lushoto (asilimia 0.4 kwa kila moja).

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Kaskazini Unguja ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki cha malaria ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha hakuna tofauti ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Wilaya za mkoa wa Kaskazini Unguja.

MKOA WA KUSINI UNGUJA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5




Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Kusini Unguja ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki cha malaria ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha hakuna tofauti ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Wilaya za mkoa wa Kusini Unguja.

**MKOA WA MJINI MAGHARIBI  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5**



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Mjini Magharibi ni asilimia moja (1). Kiwango hiki cha malaria ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Matokeo yanaonesha viwango vya malaria vinatofautiana miongoni mwa Wilaya za mkoa wa Mjini Magharibi. Kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kipo katika Wilaya ya Magharibi A (asilimia 0.7) na kiwango kidogo kipo katika Wilaya ya Magharibi B (asilimia 0.5).


MKOA WA KASKAZINI PEMBA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Kaskazini Pemba ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki cha malaria ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha hakuna tofauti ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Wilaya za mkoa wa Kaskazini Pemba.



MKOA WA KUSINI PEMBA  
KIWANGO CHA MALARIA KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA 5



Kiwango cha malaria kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mkoa wa Kusini Pemba ni chini ya asilimia moja. Kiwango hiki cha malaria ni kidogo ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 7.3. Takwimu zinaonesha hakuna tofauti ya viwango vya malaria miongoni mwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano baina ya Wilaya za mkoa wa Kusini Pemba.

# Mikakati ya Kudhibiti Malaria kwa Tanzania Bara

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatekeleza mpango wa Taifa wa kudhibiti malaria kupitia Mpango Mkakati wa Miaka mitano ulioanza mwaka 2015-2020. Lengo kuu ni kupunguza maambukizi ya malaria katika Jamii kutoka asilimia 10 mwaka 2011/12 hadi 5% (2016), hatimaye kufikia asilimia chini ya moja mwaka 2020.

Mikakati ya kudhibiti malaria inayotekelezwa inalenga kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kujikinga na maambukizi dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kutumia afua mbalimbali, pia kuhakikisha upatikanaji wa dawa ya mseto ya kutibu wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini:

## 1. Afua zinazotekelezwa ili kuikinga jamii dhidi ya maambukizi ya malaria

Afua zinazotekelezwa ili kujikinga dhidi ya malaria zinalenga;

- Kusambaza na kuongeza matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu katika kaya;
- Kugawa vyandarua kwa akina mama wajawazito wakati wa hudhurio la kwanza la kliniki ya wajawazito na watoto wachanga wakati wa hudhurio la chanjo ya surua wakiwa na miezi tisa. Lengo ni kuhakikisha makundi haya yanayoweza kupata athari kubwa za malaria yanatumia vyandarua kujikinga dhidi ya ugonjwa wa malaria;
- Kugawa vyandarua kupitia wanafunzi mashuleni katika mikoa 14 yenye maambukizi makubwa ya malaria: Kigoma, Geita, Kagera, Tabora, Mwanza, Mara, Shinyanga, Pwani, Morogoro, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Simiyu na Katavi. Mpango huu unatekelezwa ili kuhakikisha viwango vya umiliki na matumizi ya vyandarua katika kaya yanakuwa endelevu;
- Kunyunyizia dawa ya ukoko majumbani katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita na Mara;
- Kuangamiza viluwiluwi vya mbu kwa kutumia viuadudu vya kibaiolojia (Biolarvicide). Lengo ni kukabiliana na mbu katika mazalia yake kwa kulenga viluwiluwi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba, imejenga kiwanda kwa ajili ya kutengeneza viuadudu hivyo vya kibaiolojia.

## 2. Tiba sahihi ya malaria

Lengo la mkakati huu ni kuhakikisha wagonjwa wanaodhaniwa kuwa na malaria wanapata huduma mapema na kufanyiwa vipimo kwa kutumia aidha vitendanishi (mRDT) au Hadubini ili kujua kama wana malaria, na wale wanaogunduliwa kuwa wana malaria wanapata tiba sahihi kwa kutumia dawa zinazopendekezwa kwa wakati mwafaka ili kupunguza uwezekano wa kuingia kwenye malaria kali na vifo.

- Mwongozo wa kutibu ugonjwa wa Malaria nchini ulitayarishwa mwaka 2006 na kupendekeza matumizi ya dawa ya Mseto ya Malaria “Artemether-Lumefantrine” (Alu) kama chaguo la kwanza la tiba ya Malaria isiyo kali. Ulireejewa tena mwaka 2014 ili kuuboresha zaidi kulingana na mabadiliko yaliyojitokeza hususani matumizi ya kipimo cha mRDT na *Injectable artesunate* kama chaguo la kwanza kwa tiba ya malaria kali.

